# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO (ORFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuijaalia nchi yetu kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufika leo katika Baraza hili, tukiwa wazima na wenye afya njema. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kuidumisha amani na utulivu katika nchi yetu ili tuweze kuendelea kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuendelea kutoa shukurani za dhati na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa umahiri wake katika kuendelea kuiongoza nchi yetu na kuweza kutekeleza ahadi alizozitoa kwa wananchi. Pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa ufanisi na mafanikio makubwa tangu alipoanza kuiongoza nchi yetu. Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman pamoja na Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa ukaribu mkubwa katika kufanikisha majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kuendelea kutuongoza vyema na tukaweza kufanikisha majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa. Ni dhahiri kuwa, mashirikiano na uongozi wenu katika Baraza hili unapelekea kufanikisha shughuli zetu kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuendelea napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti ambao tulishirikiana kwa pamoja katika kufanikisha kazi zetu. Nikiri kuwa, Wajumbe hawa wamekuwa msaada mkubwa kwangu katika kazi zetu na wameonesha weledi na juhudi za hali ya juu katika kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM). Aidha, naishukuru Sekeretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati kutupatia ushauri wa kitaalamu uliyofanikisha utekelezaji wa kazi zetu. Napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Rukia Omar Ramadhan | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Suleiman Masoud Makame | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Yussuf Hassan Iddi | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Abass Vuai Moh'd | Katibu |
| 10. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 11. | Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 12. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii imezingatia matakwa ya Kanuni ya 101(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2024) ambayo inaitaka Kamati kujadili makadirio ya Wizara kabla ya kujadiliwa na Baraza. Hivyo, Kamati ilijadili makadirio ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) kwa kupitia mafungu saba ambayo ni Fungu F01 – Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Fungu F02 - Mfuko Mkuu wa Serikali, Fungu F03 - Tume ya Mipango, Fungu F04 – Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Fungu F05 - Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu F06 - Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, na Fungu F07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kujadiliana na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) kwa mwaka wa fedha ya 2025/2026 sambamba na utekelezaji wa

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha ya 2024/2025.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 0FISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO (ORFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kwamba, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) ilikadiria kukusanya TZS 4,901.69 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, Ofisi imekusanya TZS 2,045.83 bilioni sawa na asilimia 42 ya makadirio ya mwaka. Kwa kuwa kiwango kilichokusanywa si cha kuridhisha na hasa ukizingatia kwamba, mapato kutoka vyanzo vya mikopo na misaada kutoka Washirika wa Maendeleo yamefikia asilimia 20 na Gawio la Mashirika yamefikia asilimia 24, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM), kuongeza juhudi ya ukusanyaji wa mapato kwa kipindi kilichobakia sambamba na kuweka mikakati mahsusi ya kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi katika mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) ilikadiria kutumia TZS 1,133.21 bilioni. Hadi kufikia Machi, 2025, TZS 588.074 bilioni zimetumika sawa na asilimia 52 ya makadirio ya mwaka. Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, katika kufanikisha shughuli zake, kuendelea kufanya matumizi kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali katika utekelezaji wa miradi, utekelezaji wa kazi za kawaida za Ofisi pamoja na shughuli nyengine. Kufanya hivyo kutasaidia katika kuimarisha utendaji kazi wa Serikali na kuleta msukumo wa kukamilisha shughuli zilizopangwa kwa muda uliokusudiwa na kwa ufanisi mkubwa.

## TATHMINI YA MWELEKEO WA BAJETI YA 0FISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO (ORFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) inakadiriwa kukusanya TZS 6,506.534 bilioni. Mapato hayo ni ongezeko la asilimia 33 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya TZS 4,901.691 bilioni yaliyopangwa kwa mwaka 2024/2025. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hili la mapato na ni matumaini ya Kamati yetu, Serikali itajipanga vyema ili kuhakikisha inafanikiwa kuyafikia makadirio haya. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na juhudi za kujenga uwezo wake wa ndani na kuweza kujitegemea ili kuendelea kupunguza utegemezi kutoka kwa

wadau wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kuongezeka kwa makadirio ya mapato ni dalili njema kwani inaonesha Serikali imejidhatiti katika kusimamia vyema makusanyo yake kupitia mifumo iliyoimarishwa pamoja na kudhibiti upotevu wa mapato kwa kuhakikisha inaziba mianya ya uvujaji wa mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) inakadiriwa kutumia TZS 1,570.56 bilioni. Makadirio hayo ni ongezeko la asilimia 39 ikilinganishwa na makadirio ya kutumia TZS 1,133.21 bilioni yaliyopangwa katika mwaka 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Fungu la Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango (F01), jumla ya fedha zilizokadiriwa kutumika kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni TZS 865.540 bilioni. Kiasi hichi kinaonyesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 30 ikilinganishwa na makadirio ya TZS 665.392 bilioni kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kuzingatia ongezeko hili, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa ongezeko hilo linaendana na usimamizi madhubuti wa rasilimali, utekelezaji wa vipaumbele, na upimaji wa matokeo kwa lengo la kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa vipaumbele vya bajeti hii ni pamoja na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali yakiwemo mapato ya ndani na mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kamati inaunga mkono utekelezaji wa vipaumbele hivi sambamba na kuishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) kuendelea kusimamia mifumo ya ukusanyaji wa mapato, kujenga uwezo wa watendaji wanaosimamia mifumo hiyo pamoja na kuendelea kuimarisha taasisi zinazohusika na ukusanyaji mapato ili kudhibiti upotevu wa mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu F02 - Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026, fedha zilizotengwa zimeongezeka kutoka TZS 416.897 bilioni na kufikia TZS 641.350 bilioni. Kamati inakubaliana na ongezeko hili pamoja na kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba matumizi ya fedha hizi yanakwenda sambamba na malengo ya Serikali ikiwemo kufanya malipo ya matumizi maalum ya Serikali pamoja na kufanya malipo ya madeni ya Serikali. Kwa upande mwengine, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) kupitia fungu hili, kuweka mkazo zaidi katika miradi ambayo haijakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia Fungu F03 - Tume ya Mipango, jumla ya TZS 20.380 bilioni zimekadiriwa kutumika kwa mwaka 2025/2026. Kamati inaafikiana na makadirio hayo sambamba na kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba malengo yote ya Tume ya Mipango yaliyopangwa katika bajeti hii yanatekelezwa kwa ufanisi na kuleta mafanikio yaliyokusudiwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya Kitaifa na Miradi ya Maendeleo pamoja na kuchukua hatua zinazostahiki ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu F04 linalosimamiwa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali linakadiriwa kukusanya jumla ya TZS 180.3 milioni ambazo zitachangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, kwa upande wa matumizi fungu hilo linakadiriwa kutumia jumla ya TZS 11.607 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwani yatawezesha Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yake hususan ufanyaji wa tafiti mbali mbali zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2025/2026 kama vile utafiti wa kaya kuhusu udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu zitakazopatikana kupitia utafiti huo, zitaisaidia Serikali katika kupanga mikakati ya kuyanusuru makundi hayo muhimu kutokana na vitendo vya udhalilishaji. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi tafiti zinazofanyika ili lengo na tija za tafiti hizo zitimie.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Fungu F05 ambalo linasimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali, kwa mwaka fedha 2025/2026 linakadiriwa kukusanya jumla TZS 2.980 trilioni na kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, fungu hilo linakadiriwa kutumia jumla ya TZS 17.589 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za msingi ikiwemo ya usimamizi wa hazina na kuhakikisha kunakuwepo na usimamizi mzuri wa matumizi pamoja na utoaji taarifa za mwenendo wa fedha katika Mfuko Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inayaafiki makadirio haya sambamba na kuishauri Serikali kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha, hususan mifumo ya TEHAMA, ili kuongeza uwazi, ufanisi na kupunguza mianya ya upotevu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Fungu 06 ambalo linasimamiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kwa mwaka fedha 2025/2026 limekadiriwa kutumia TZS 6.479 bilioni ili

kuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kuimarisha huduma za ukaguzi wa ndani, kuimarisha ubora na ufanisi katika kazi za uchunguzi na kuhamasisha ufuatiliaji wa viwango vya ubora katika kazi za ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu F07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina limekadiriwa kukusanya TZS 28.5 bilioni kupitia Idara ya Usimamizi wa Mashirika pamoja na Idara ya Usimamizi wa Mali za Umma. Kwa upande wa Matumizi, Fungu F07 limekadiria kutumia jumla ya TZS 7.609 bilioni. Kamati inaishauri Ofisi ya Msajili wa Hazina kuhakikisha fedha walizotengewa wanazitumia vyema katika kutekeleza programu zao ikiwemo kufanya usimamizi mzuri wa mali za umma pamoja na kuhakikisha uwekezaji wa mashirika ya umma unaimarika kwa vile ni lengo la Serikali kuimarisha ufanisi wa sekta za umma ambazo zinachukua nafasi kubwa katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu.

## TATHMINI YA MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAYOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO (ORFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango imepanga kutekeleza programu 6 pamoja na miradi 6 ya maendeleo yenye thamani ya TZS 707.017 bilioni ambayo imelenga kusaidia kukuza ajira, kuimarisha hali za wananchi pamoja na kuchangia katika Pato la Taifa. Kamati inaishauri Serikali kuweka mipango madhubuti ili kuhakikisha kuwa miradi na programu zote zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2025/2026 inakamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti wakati inafuatilia utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 imegundua kuwepo kwa baadhi ya miradi na programu zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huo haukuwa wa kuridhisha kutokana na changamoto mbali mbali hususan ya uhaba wa upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande mwengine, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati kwa taasisi zote zinazokamilisha taratibu za maombi ya fedha. Hii ni kutokana na uingizwaji wa fedha kuwa wakusuasua katika baadhi ya miradi katika mwaka wa fedha 2024/2025 na wakati mwengine hazipatikani kabisa. Mathalan, katika Mradi wa Vituo vya Mafunzo kwa Vijana Awamu ya Pili na Programu ya Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Afya

ya Msingi kumekuwepo na changamoto ya kukosekana kwa fedha za utekelezaji. Hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha fedha zinazopangwa katika bajeti zinapatikana kwa wakati ili kuweza kukamilisha miradi kwa muda uliokusudiwa. Kukosekana kwa fedha hizo, kunazorotesha utekelezaji wa miradi hiyo.

## TATHMINI YA MWELEKEO WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA 0FISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO (ORFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imepangiwa kukusanya TZS 1,257.240 bilioni, sawa na ongezeko la asilimia 49 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya TZS 845.979 bilioni katika mwaka 2024/2025. Aidha, ZRA inatarajiwa kupata ruzuku ya TZS 30.156 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya mishahara na uendeshaji wa ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na kuhakikisha inavuka lengo la makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe. Kwanza, ZRA inapaswa kuendelea kuimarisha mifumo ya kidijitali ili kurahisisha ulipaji wa kodi, ukusanyaji wa takwimu sahihi na ufuatiliaji wa walipa kodi kwa wakati. Pili, ni muhimu kupanua wigo wa walipa kodi kwa kuandikisha wafanyabiashara wadogo, wa kati na sekta zisizo rasmi, ili kuwaingiza katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi. Tatu, Kamati inaishauri ZRA kuimarisha udhibiti wa ukwepaji kodi kwa kuimarisha vitengo vya ukaguzi na ufuatiliaji hasa katika maeneo ya forodha na bidhaa zisizo na nyaraka halali. Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa ushirikiano wa karibu na taasisi nyingine za Serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Bandari, na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ili kuwezesha mabadilishano ya taarifa muhimu kwa ajili ya kudhibiti mapato. Nne, kuimarisha ufanisi wa ufanyaji kazi na maadili ya watumishi wa ZRA kutachangia kuongeza imani ya walipa kodi na kuimarisha makusanyo ya mapato ya Serikali.

### Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, TRA Zanzibar imepangiwa kukusanya TZS 825.769 bilioni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 38 ikilinganishwa na makadirio ya TZS 600.082 bilioni kwa mwaka wa 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** TRA Zanzibar inaweza kufikia mafanikio na kuvuka lengo la mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kupitia matumizi ya teknolojia ya kisasa inayowezesha ufuatiliaji wa miamala na uwazi wa mapato. Ni muhimu pia kuwekeza katika elimu ya walipakodi ili kuongeza uelewa na kujenga utamaduni wa ulipaji kodi kwa hiari miongoni mwa wananchi na wafanyabiashara. Vilevile, kushirikiana kwa karibu na taasisi nyingine za Serikali kama ZRA, Shirika la Bandari Zanzibar, kutasaidia kuzuia upotevu wa mapato. Hatua hizi zitaimarisha ufanisi wa TRA na kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake kwa mafanikio na ufanisi mkubwa.

### Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar (ZPPRA)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar (ZPPRA) imepanga kukusanya TZS 1.175 bilioni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 18 ikilinganishwa na makadirio ya TZS 989 milioni kwa mwaka uliotangulia. Kwa upande wa matumizi, Mamlaka imekadiriwa kutumia TZS 3.274 bilioni ambazo ni ruzuku kutoka Serikalini, ambapo TZS 1.780 bilioni zitatumika kwa malipo ya mishahara na TZS 1.493 bilioni kwa shughuli mbali mbali za ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kuhakikisha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar (ZPPRA) inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuvuka lengo la mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati inapendekeza Mamlaka kuchukua hatua zifuatazo: Kwanza, Mamlaka iendelee kusimamia kwa umakini utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kupitia ukaguzi wa mara kwa mara katika taasisi nunuzi, uchunguzi wa manunuzi na ufuatiliaji wa mikataba ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma. Pili, utoaji wa mafunzo kwa maafisa manunuzi, maafisa masuuli, wajumbe wa bodi za zabuni na watoa huduma kuhusu sheria, kanuni na nyaraka za ununuzi wa umma ni muhimu katika kujenga uwezo wa watendaji na kuhakikisha utii wa sheria. Tatu, ZPPRA inapaswa kuwekeza katika

mifumo ya kidijitali kwa ajili ya kusimamia manunuzi ya umma ili kuongeza uwazi, kupunguza mianya ya upotevu wa fedha na kurahisisha ukusanyaji wa taarifa.

## Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ZSSF inatarajia kukusanya jumla ya TZS 360.50 bilioni kutoka kwenye michango ya wanachama (TZS 206.74 bilioni) na mapato yatokanayo na uwekezaji na vyanzo vingine (TZS 153.76 bilioni). Kwa upande wa matumizi, kiasi hicho hicho cha TZS 360.50 bilioni kitatumika kugharamia mafao (TZS 117.03 bilioni), usimamizi wa miradi na uwekezaji (TZS 226.13 bilioni), pamoja na gharama za uendeshaji (TZS 17.34 bilioni). Zaidi ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku, ZSSF imepanga kuendelea kuwekeza kwenye hatifungani, benki na kutoa mikopo kwa baadhi ya taasisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini ZSSF inaweza kufanikisha malengo yake ya mapato kwa kupanua wigo wa wanachama, kuimarisha ukusanyaji wa michango, kufanya uwekezaji wenye tija, na kuimarisha mifumo ya usimamizi, uwajibikaji, na ufuatiliaji wa fedha.

## Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) inatarajiwa kuongeza mapato yake hadi kufikia TZS 277.2 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 38 ukilinganisha na TZS 201.4 bilioni katika mwaka 2024/2025. Kuongezeka kwa mapato haya kunatokana na kuongezeka kwa utoaji wa mikopo na ufunguaji wa matawi mapya. Kwa upande wa matumizi, PBZ imepanga kutumia TZS 156.7 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 43 ukilinganisha na TZS 109.3 bilioni kwa mwaka 2024/2025. Ongezeko hili limetokana na PBZ kupanga kuanzisha matawi mapya na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** PBZ inaweza kufanikisha utekelezaji wa shughuli zake na kuvuka lengo la mapato kwa kuimarisha huduma za kidijitali, uwekezaji katika mifumo ya TEHAMA ili kuongeza usalama wa kimtandao, kuendelea kutoa mikopo yenye tija na yenye viwango rafiki kwa wananchi na wafanyabiashara wadogo na wa kati, jambo ambalo litasaidia

kukuza uchumi na kuongeza mapato ya riba kwa benki, na kuimarisha ufanisi wa ndani kwa kuhakikisha watumishi wana uwezo na motisha wa kutosha, huku pia ikizingatia usimamizi bora wa matumizi ya fedha.

### Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) linatarajia kukusanya TZS 57.3 bilioni kwa mwaka 2025/2026 kupitia mikakati ya kutoa elimu na kujitangaza kwa wananchi na taasisi mbali mbali, pamoja na kuimarisha ushirikiano na mawakala, madalali, na mabenki kupitia mfumo wa "Bancassurance." Kwa upande wa matumizi, Shirika linakadiriwa kutumia TZS 40.1 bilioni, ikiwa ni pamoja na TZS 13.7 bilioni kwa matumizi ya kawaida, TZS 4.3 bilioni kwa ununuzi wa vitendea kazi, TZS 13.6 bilioni kwa malipo ya madai kwa wateja waliyoathirika, na TZS 8.5 bilioni kwa malipo ya ujira kwa mawakala na madalali.

**Mheshimiwa Spika,** Ili Shirika liweze kufikia ufanisi na kuvuka malengo yake ya mapato kwa mwaka 2025/2026, linapaswa kutoa huduma bora zaidi ili kuyashinda makampuni mengine shindani na kuvuta wateja wapya.

### Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ZIAAT inatarajia kukusanya TZS 657.87 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, ikiwa ni pamoja na Ada ya Usajili, Utambuzi, Leseni, Mwaka, na Ada ya Mafunzo. Kwa upande wa matumizi, ZIAAT imepanga kutumia TZS 2.492 bilioni kutoka Serikalini kama ruzuku. Kati ya fedha hizo, TZS 418 milioni zitatumika kwa mishahara, na TZS 2.07 bilioni kwa shughuli za uendeshaji ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** Ili ZIAAT iweze kufikia ufanisi na kuvuka malengo yake ya mapato kwa mwaka 2025/2026, ni muhimu ZIAAT kuwekeza katika majukwaa ya kidijitali ili kurahisisha utoaji wa huduma, ikiwa ni pamoja na usajili, malipo ya ada, na upatikanaji wa taarifa kwa wanachama. Hii pia itawawezesha wanachama kupata huduma kwa urahisi na haraka, jambo ambalo litavutia wanachama zaidi.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Bajeti kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) kwa mwaka wa Fedha 2025/2026. Kipekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa umakini wakati nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati yangu imejadili kwa kina na kuyakubali makadairio ya mapato na matumizi kwa mafungu yote saba (7) ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 sambamba na shabaha zake. Naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili bajeti hii, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waipitishe ili kuwezesha kutekelezwa kwa shughuli za Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM) zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, na kwa niaba ya Kamati ya Bajeti naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………………….....

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**